



The Ark
Shofar

The Echoes of His Mighty Doings **Rev 12:11**

Come and See what the Lord has Done

The Ark Fellowship Magazine
The Ark Testimonies Magazine

Surreal
Zaburi 126:1



Testimony

THE JOB I PRAYED FOR THE GOD WHO ANSWERED LOUDLY

Ask, and it shall be given to you” – Matthew 7:7

I have a testimony.

I HAVE BEEN PRAYING FOR A JOB FOR THREE YEARS NOW.

Mwezi wa kwanza, taasisi flani ilitangaza kazi. Vigezo walivyoandika sikuwa navyo, ila kazi hiyo ilikuwa ya fani yangu. I prayed and applied. Mwezi wa tatu walituita kwenye interview, and my name was on the list. We did both the written and oral interview that same month.

Majibu yalitoka juzi wakati tupo kwenye day 2 ya dry fast. Na cha kushangaza: jina langu halikuwepo kati ya walioitwa kuchukua barua za kazi. **I cried. Nikamuuliza Mungu, “Kwanini?”**

Akanijibu: “Don't break your fast. Maliza maombi and I will show you who I am. Trust Me even in the storm.”

Nikamaliza mfungo asubuhi ya Jumamosi, nikaendelea na shukrani.

Walioitwa kuchukua barua waliambiwa wafike Jumatano ya wiki hiyo. Jumatatu, as I was leaving my activities, ndani yangu nikasikia Mungu akisema:

“Esther alifunga siku tatu na hakukaa tu, aliingia kwa mfalme kinyume cha utaratibu. Nenda Dodoma!”

Nilichukua vyeti vyangu usiku huo huo, nikaondoka kwenda Dodoma. Njiani nilikuwa nikiomba kibali na kutuma malaika kwenye ile taasisi.

Nilifika Dodoma saa nne asubuhi Jumanne. Nikakwenda moja kwa moja hadi kwenye taasisi. Nikaomba kuonana na wakuu wa taasisi hiyo. Nilipewa nafasi,

NIKAWAULIZA:

“Mbona tulikuwa wasichana saba kwenye usaili na sita wameitwa, ila mimi pekee sijaitwa?”

Wakasema ushindani ulikuwa mkubwa, lakini zikitokea fursa nyingine, tutakujulisha. Nikashukuru na kuondoka. Asubuhi ya siku inayofuata ambao ndio wenzangu walikuwa wanachukua barua nikaanza safari ya kurudi kwasababu sikupata any feedback inayonilazimu kubaki.

Fika ofisini haraka

Nikashuka kwenye gari, nikachukua usafiri mwingine kurudi. Nilipofika, yule mama niliyemwona jana akaniambia:

“HUYO MUNGU UNAYEMWOMBA NI MKALI SANA. YOU ARE LUCKY. MSHUKURU MUNGU.”

Akanipa documents zile zile ambazo wenzangu walipewa. Alhamisi nikapewa barua ya kazi. Na kituo nilichopangiwa kazi ndicho nilichokuwa najitolea. Nakumbuka... kila siku nikiingia kazini pale nilipokuwa najitolea, niliombea kiti changu, nilikanyaga kwa miguu ardhi pale ninapokaa, nikiamuru ardhi itii neno la bwana.

MUNGU AMENIJIBU.

Ninarudi kwenye ardhi niliyoombea, sasa nikiwa na barua ya kuripoti kituo cha kazi.

Miaka mitatu ya kutafuta kazi, taasisi hiyo haikuwahi kutangaza nafasi yoyote.
Still, I prayed. I praised. I trusted God.

Niliwahi kujiandikia barua ya kupangiwa kituo cha kazi, nikaweka kwenye bahasha. Nikaamka saa tisa usiku navaa nguo za taasisi hiyo. Namsifu Mungu kana kwamba nimeshapata kazi.

**MUNGU AMENIPA TAASISI ILE ILE.
KITUO KILE KILE.**

Matthew 7:7
Ask and you shall receive."

At the right time, He has done it.
Hachelewi wala hawahi.

Glory to God!

Testimony

SHALOM SIS

I hope your doing great nina mambo mengi ya **kumshuhudia Mungu**, amemponya baba yangu alikua anasumbuliwa na Miguu alikua hawez hata kuvaa viatu pia aliambiwa anatezi dume ila Mungu amefanya mambo makubwa sana katika familia yetu, hajaishia hapo ameenda beyond my expectations I have been unemployed for a long time, kwenye maombi yale ya siku tatu kavu nilimwambia Mungu nimezunguka sana kwenye jangwa inatosha.

Mungu amenionekania nimekuja kutoa **shuhuda** next week I'm going to sign a contract of an international **NGO**, yale maombi ya protocol breaking tuliyoyaomba **Yohana 5:7**.

I prayed for an international job zile ambazo wanasema lazima uwe na mtu akuunganishe au umjue mtu ndo upate, **I told God you will be my connector I don't have anyone rather than you, and look what he did he did beyond my thinking**, I will surely come back with my thanks giving offering na praise song

Gods time is the best time, hachelewi wala hawai anajibu kwa wakati wake.

etc

Testimony

SHALOOM MTUMISHI WA MUNGU

Kwa kweli namshukuru MUNGU Sana kwa ajili yako nilikuujia na shida yangu ya ugum wa biashara

Kwamba, nafungua biashara nafunga, nikafunga saloon na duka nikawa natoka sijauza hata Mia biashara zote mbili yaani hata mtu kuja kuulizia tu hamna.

Nilivokueleza unaniambia niwe najiunga maombi kwa **link** zenu na unanipa muongozo namna ya kujiunga kwa kweli nilitii **saa Tisa usiku** naamka na hii madhabau na **Saa nne pia** nashiriki, Ni wiki na nusu tu mpaka Sasa tangu nimeshiriki kikamilifu kwa kweli **Saloon** naanza kuona watu na nawahudumia na **Dukani** pia nimeanza kuona watu wa kununua hata wa kuulizia kwa kweli nimeona hatua jamani **namshukuru MUNGU Sana**

Napia tangu nimeanza maombi ya hii madhabau niliua **nyoka getini** kwangu usiku natoka kwenye biashara yangu narudi dukani nikakutana na nyoka **getini kaganda** hawezi hata kutembea nilimua Mimi mwenyewe, Leo nakuja **Saloon** pia namwaga maji ya usafi mbele naona **Nyoka** tena kafa kwa **kweli nashangaa MUNGU mno.**

Testimony

SHALOM MY SIS

Namshukuru Mungu kwa ukuu wake, namshukru Mungu wangu kwa kuniurumia na kuniponya hermoloids yaani ilikuwa imevimba sana kwenye maombi ya tatu kavu mliomba kwa ajili ya wenye hermoloids kwa kweli namtukuza Mungu baada ya mfungo kuna siku nilisikia maumivu makali mnooo.

Nikaomba nikamwambia Mungu naomba unisaidie maumivu yaishe na nisiumwe tena huu ugonjwa. Baada ya kumaliza maombi yaani haijachukua hata **dk20** maumivu yakawa yameisha kabisa na uvimbe umepungua.

Hakika narudisha utukufu kwa Mungu kwa sababu yeye yupo na anasikia na kujibu, nafunika ushuhuda wangu kwa **damu ya Yesu** Mungu awabariki sana viongozi wetu.

Testimony

SHALOM SIS

Ni viwango hadi viwango utukufu hadi utukufu kwakweli nakosa lugha nzuri ya kushukuru.

Huyu Mungu amekuwa mwema kila siku Jana maombi ya watu wasiokuwa na chochote niliomba Mungu anisaidie nipate pesa sababu mambo yapo mengi ya kufanya kama nyie viongozi mlivotuambia,

Nikamwambia Mungu nisaidie nikamilishe ahadi yangu ya **partner** mapema ili vitu viendelee **guess what** Bwana kanipaaisee sifa kwa BWANA mbarikiwe viongozi wetu yaani nilikuwa sioni mpenyo wowote Mungu kaniletea mteja mmoja tu nyie tusichoke kuomba.

Yupo Mungu asikiaye Maombi yetu.

Testimony

SHALOM SIS

Mungu wetu ni mkuu sanaa sanaa, Leo kwenye maombi ya saa nne ya **Business alter** nimepata kumuona Mungu

Kwa kupitia maombi ya leo nilikuwa natamka wateja wote walio mashariki na magharibi kaskazini na kusini nguvu ya Mungu ikawaguse mje dukani kwangu.

Hakika sauti ya bwana inanguvu baada tuu ya kumaliza maombi **saa sita** mchana **dada wa dukani** (niliemwajiri) ananipigia sim ananiambia hapa dukani kaja mteja anataka **pair 70** za slippers kwa bei ya jumla

Oooh Lord my God see our God alivyomtam , Mungu ameniletea mteja from no where na mimi biashara yangu imebase sana mtandaoni hamna mteja anaenda pale physicaly kama hajapiga sim from business platform (instagram) , huyu mteja kaja from no where jamani na ameacha mauzo ya maana skutegemea leo kama ningepata iyo pesa. Mungu wetu ukimwita anaitika jamani tena kwa namna yake ya kipekeee , niliahidi nitakuja na ushuhuda wenye nguvu ili nimshinde adui , oooh Yesu kanitendea na kwa mauzo ya leo ntatoa sadaka yangu izidi kuwezesha iyo safari ya watumishi wanaoenda kuhudumu Arusha

Hakika Mungu atazidi kutupa financial breakthrough ili nasisi tuweze kusongesha injili yake mbelee

The Echoes of His Mighty Doings Rev 12:11

Come and See what the Lord has Done



- *The Ark Fellowship Magazine*
- *The Ark Testimonies Magazine*